HakE Muhtasari Na. 07K, 2018

Muhtasari wa Tathmini Ya Mafunzo Na Ushirikishwaji Wa Wanafunzi Wenye Changamoto Za Uoni Katika Shule Jumuishi Nchini Tanzania

S.L.P 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2151852 or 3
Nukushi: +255 (22) 2152449
Barua pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

February, 2018

Tathmini Ya Mafunzo Na Ushirikishwaji Wa Wanafunzi Wenye Changamoto Za Uoni Katika Shule Jumuishi Nchini Tanzania

1.0. Utangulizi na Maudhui ya Tafiti

HakiElimu inatekeleza Mpango Kazi mpya (2017-2021) ambao pamoja na mambo mengine umejikita katika kuhamasisha uboreshwaji wa mazingira ya kujifunza na kufundisha katika shule jumuishi. HakiElimu ilianza utekelezaji wa Mpango Kazi huu mnamo mwaka 2017 kwa kufanya utafiti juu ya mazingira ya shule jumuishi na hasa kuangalia "namna wanafunzi wenye changamoto za uoni wanavyoshiriki na kujifunza katika shule jumuishi nchini Tanzania''. Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kutathmini kama mazingira ya shule jumuishi yanakidhi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na kama sera na mikakati ya elimu inakidhi mahitaji tofauti ya wanafunzi wakati wa kujifunza na kufundishwa.

2.0. Methodolojia na washiriki wa utafiti

Utafiti huu umefanyika katika shule za msingi na sekondari za serikali zenye wanafunzi walio na changamoto za uoni katika mikoa tisa ya Tanzania bara ikiwemo; Dodoma, Iringa, Lindi, Morogoro, Mwanza Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. Walioshiriki katika utafiti huu ni pamoja na wanafunzi wa shule hizo za msingi na sekondari walio na changamoto za uoni na wasiokuwa na changamoto za uoni, walimu wa madarasa, walimu wakuu, wazazi, walezi wa wanafunzi walio na changamoto za uoni na maafisa elimu. Katika kuhakikisha ukusanyaji wa taarifa unaboreshwa njia mchanganyiko zilitumika katika kukusanya taarifa, yaani mbinu ya uchambuzi wa ubora na uchambuzi wa kitakwimu (qualitative and quantitative).

3.0. Muhtasari wa matokeo muhimu ya utafiti

Matokeo haya ya utafiti yamejikita katika kuchambua maeneo makuu matano ambayo yametokana na malengo ya utafiti. Maeneo haya ni pamoja na kutathmini mazingira na vifaa vya

kujifunzia kwa wanafunzi wenye changamoto za uoni; usaidizi wa walimu katika kujifunza kwa watoto wenye changamoto za uoni; namna wanafunzi wenye changamoto za uoni wanavyojifunza ujuzi unaohitajika pamoja na ufaulu wao; ushiriki wa wanafunzi wenye changamoto ya uoni katika masuala ya kijamii katika shule jumuishi na uelewa wa maafisa elimu juu ya Mkakati wa kitaifa juu ya Elimu Jumuishi.

3.1. Mazingira na vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi wenye changamoto ya uoni

Sehemu hii iliangalia namna mazingira ya kujifunzia yanavyoweza kuwasaidia wanafunzi wenye changamoto za uoni katika kujifunza kwa kuangalia maeneo matatu yaani;-

- Mazingira ya kufundishia na kujifunzia
- Ubora na kujitosheleza kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia
- Kuwawezesha wanafunzi wenye changamoto za uoni katika kutumia vifaa vya kujifunzia na namna bora ya kuishi katika mazingira jumuishi.

3.1.1. Mazingira ya Kujifunzia

3.1.1.1. Urahisi wa kutembea ndani ya shule

- Kulingana na utafiti, wanafunzi wengi wenye changamoto za uoni walikiri kutoridhishwa na mazingira ya kujifunzia ambayo si rafiki na yanawazuia kutembea kwa uhuru. Mazingira hayo yasiyo rafiki ni pamoja na barabara mbaya, vyoo visivyo na miundombinu ya kukidhi mahitaji yao na umbali mrefu kutoka katika mabwenihadi madarasani.

- Walimu (ambao wengi hawana changamoto za uoni) walitoa maoni tofauti na yale yaliyotolewa na wanafunzi wenye changamoto za uoni.

Asilimia 81 ya walimu walisema kuwa wanafunzi walio na changamoto za uoni wanauwezo wa kutembea katika maeneo ya shule bila vikwazo.

3.1.1.2. Mpangilio wa darasa

- Asilimia 66 ya walimu walieleza kuwa mpangilio wa darasa hauridhishi na ni kikwazo katika maendeleo, ushiriki na kujifunza kwa wanafunzi walio na changamoto ya uoni.

3.1.1.3. Miundombinu ya shule

- Asilimia 69 ya walimu walikiri kwamba miundombinu ya shule ikiwemo madarasa, vyoo, barabara n.k, haijajengwa kwa kunzingatia mahitaji ya wanzafunzi wenye changamoto za uoni.

- Asilimia 81 ya walimu walipendekeza kuwa wanafunzi wenye changamoto za uoni watapata elimu stahiki wakiwa katika shule maalum kuliko katika shule jumuishi.

3.1.2. Kujitosheleza, ubora na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia

Katika kufanya tathmini ya kujitosheleza na ubora wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule jumuishi, yafuatayo yalibainishwa;-

- Asilimia 87 na asilimia 60 ya wanafunzi walio na changamoto za uoni walieleza kwamba mahitaji maalum ya kujifunzia kwa watoto wenye changamoto za uoni hayakidhi mahitaji ya kundi hilo.

- Ubora na ubunifu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia haviendani na mahitaji ya kundi la wanafunzi wenye changamoto za uoni kwani

baadhi ya vitabu vina majalada yenye picha kama vile vimetengenezwa kwa ajili ya wanafunzi wasio na chanagamoto za uoni. Pia vitabu vimetengenezwa na majalada yasiyo imara hivyo kusababisha vitabu hivyo kuharibika mapema.

- Kuna umuhimu wa kutenga na kupeleka fedha zinazokidhi mahitaji ya shule jumuishi ili kutosheleza mahitaji ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye changamoto za uoni.

- Washiriki walipoulizwa juu ya namna gani vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa watoto walio na changamoto za uoni vinavyopatikana, asilimi 55 ya walimu wakuu waliohojiwa walisema vifaa hivyo hutolewa na serikali, asilimia 34 walisema hutolewa na asasi za kiraia na asilimia 10 walisema vinatolewa na watu binafsi.

3.2 Walimu wanavyofundisha wanafunzi walio na changamoto za uoni

Sehemu hii ilitathmini ujuzi wa walimu katika kufundisha darasa jumuishi, upatikanaji wa walimu wenye ujuzi stahiki na msaada wanaotoa walimu kwa wanafunzi wenye changamoto za uoni darasani. Pia iliangalia ushiriki wa wanafunzi wenye changamoto za uoni katika masomo na namna wanafunzi hawa wanavyotendewa darasani.

3.2.1. Uwezo wa walimu kufundisha darasa jumuishi(START 080218)

Baada ya kufanya tathmini juu ya ujuzi na ufanisi wa walimu katika kufundisha katika mazingira jumuishi, yafuatayo yalibainishwa;-

- Asilimia 49 ya walimu wanaamini wana ujuzi unaotakiwa kufundisha katika darasa jumuishi, asilimia 44 wanaamini

hawana ujuzi wa kutambua na kukidhi mahitaji ya kujifunza kwa watoto wenye changamoto ya uoni na asilimia 7 hawafahamu kama wana ujuzi.

- Walimu wengi waliohojiwa walikiri kutokuwahi kuhudhuria mafunzo yoyote yanayowapa ujuzi wa kufundisha katika darasa jumuishi.

- Asilimia 33 ya wanafunzi walio na changamoto za uoni walieleza kwamba walimu hawana ujuzi maalum wa kufundisha katika darasa jumuishi. Walitoa mfano kuwa kuna baadhi ya walimu wanafundisha darasa jumuishi na hawawezi kusoma nukta nundu. Pia walieleza pamoja na kufundishwa na walimu wasiokuwa na ujuzi maalum, mitihani yao hupelekwa kusahihishwa kwa walimu wenye ujuzi maalum.

3.2.2. Upatikanaji wa walimu

- Asilimia 67 ya walimu wakuu walikiri kutokuwa na idadi ya kutosha ya walimu waliobobea katika kufundisha wanafunzi wenye changamoto za uoni na asilimia 33 walikiri kuwa na idadi inayojitosheleza.

3.2.3. Msaada wanaotoa walimu kwa wanafunzi walio na changamoto za uoni wakati wakiwa darasani

Sehemu hii ilitazama uwezo wa walimu kugundua na kushughulikia mahitaji ya wanafunzi walio na changamoto za uoni katika darasa jumuishi. Baadhi ya mambo yaliyobainishwa yalikuwa kama yafuatavyo;-

- Wakati asilimia 10 ya walimu walikiri kutoshughulikia mahitaji maalum ya wanafunzi wenye changamoto za uoni wakiwa darasani, asilimia 86 walikiri kushughulikia mahitaji ya kundi hilo na asilimia 4 hawakuwa na uhakika kama kuna umuhimu wa kushughulikia mahitaji ya kundi hilo wakiwa darasani.

- Asilimia 80 ya wanafunzi wenye changamoto za uoni

walikiri kupata msaada wa kujifunza kutoka kwa walimu wakiwa darasani. Asilimia 10 walionesha kutoridhishwa na msaada wanaopata kwa kueleza kuwa walimu wanatoa msaada sawa kwa wanafunzi bila kujali utofauti wa mahitaji kati ya wenye changamoto za uoni na wasio na changamoto za uoni.

- Asilimia 65 ya walimu walikiri kutoa msaada sawa kwa wanafunzi wote kwa kudhania kuwa wanafunzi wenye changamto ya zoni wanajifunza sawasawa na wanafunzi wengine na pia walitumia mbinu zilezile kwa makundi yote mawili wakati wa kufundisha.

- Kwa upande mwengine, asilimia 80 ya walimu walikiri kuhakikisha mpangilio wa darasa unakidhi mahitaji ya wanafunzi wenye changamoto ya uoni na pia kuhakikisha wanafunzi wanatumia vifaa vyao maalumu wakati wa kujifunza.

- Asilimia 61 ya wanafunzi walio na changamoto za uoni walisema hakuna unyanyapaa dhidi yao kutoka kwa wanafunzi wenzao.

3.3 Kujifunza na Ufaulu wa wanafunzi wenye changamoto za uoni

Eneo hili la tatu lilitathmini uwezo wa wanafunzi wenye changamoto za uoni kujifunza ujuzi unaotakiwa katika ngazi tofauti za elimu. Pia liliangalia ufaulu wa wanafunzi hawa katika mitihani ya kitaifa kwa kulinganisha na wanafunzi wenzao wasio na changamoto za uoni.

- Asilimia 75 ya walimu wanaamini wanafunzi walio na changamoto za uoni hujifunza kuandika, kusoma na hesabu ndani ya darasa jumuishi.

- Asilimia 49 ya walimu walisema wanafunzi wenye changamoto za uoni wanahitaji msaada wa ziada wakiwa darasani kwa sababu ya kushindwa kujifunza kwa haraka

kulinganisha na wanafunzi wengine.

- Asilimia 90 ya wazazi waliripoti kuridhishwa na elimu wanayopata watoto wao katika shule jumuishi.

- Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi wenye changamoto ya uoni katika mitihani ya kitaifa unatofautiana kila mwaka kwani miaka mingine ufaulu ni wa kurudhisha na miaka mingine ufauli hauridhishi.

3.4 Ushiriki wa wanafunzi wenye changamoto ya uoni katika masuala ya kijamii ndani ya shule jumuishi.

Eneo la nne liliangalia ushiriki wa wanafunzi katika kujifunza ndani ya darasa na namna wanavyoshirikiana na walimu na wanafunzi wengine katika shughuli za nje ya darasa ikiwemo michezo na burudani.

- Asilimia 43 ya walimu walieleza kuwa wanafunzi walio na changamoto za uoni hawashiriki katika matukio ya nje ya darasa na wanafunzi wengine kwa kuwa mazingira siyo rafiki.

- Asilimia 79 ya walimu walieleza kuwa, wanafunzi wenye changamoto za uoni wananyanyapaliwa na wanafunzi wenzao.

- Asilimia 52 ya wanafunzi wenye changamoto za uoni walikiri kushiriki katika shughuli za nje ya darasa kwa kushiriki michezo kama kukimbia na ‘goal ball’. (Mpira maalumu wenye kutoa mlio kwa ajili ya wasioona)

- Asilimia 48 walieleza kuwa hawashiriki katika michezo kwa sababu hakuna vifaa maalum vya kuwezesha ushiriki wao.

3.5 Uelewa wa maafisa elimu kuhusu mpango wa elimu jumuishi

Kwa kuzingatia kuwa maafisa elimu ndio watekelezaji wa sera na mipango ya elimu katika ngazi ya wilaya, watafiti walitathmini uelewa wa maafisa elimu juu ya mpango wa elimu jumuishi

- Iligundulika kuwa ijapokuwa maafisa elimu wengi wanafahamu mpango wa elimu jumuishi bado kuna wengine hawana uelewa juu ya mpango huu.

4.0. Changamoto zinazowakabili wanafunzi walio na changamoto za uoni katika shule jumuishi

Wanafunzi wenye changamoto za uoni wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo;-

- Upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia

  Upungufu wa fedha za kukidhi mahitaji ya shule jumuishi

- Kushindwa kutembea katika maeneo ya ndani ya shule kutokana na miundombinu isiyo rafiki.

- Ubora hafifu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, mfano, vitabu

- Upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha watoto wenye changamoto za uoni.

- Unyanyapaa wa wanafunzi wenye changamoto za uoni kutoka kwa walimu na wanafunzi wenzao.

- Upungufu wa wafanyakazi wa ziada shuleni kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye changamoto za uoni.

- Kutowatambua mapema wanafunzi wenye changamoto za uoni.

Washiriki walishauri kuwa changamoto zifanyiwe kazi ili kuhakikisha wanafunzi wenye changamoto za uoni wanajifunza ipasavyo katika madarasa jumuishi.

5.0. Muhtasari wa jumla wa matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaweza kujumuishwa kwa ujumla kama ifuatavyo;-

- Mazingira ya kujifunzia katika shule jumuishi siyo rafiki kwa wanafunzi wenye changamoto za uoni.
- Upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha wanafunzi wenye changamoto za uoni na vifaa vya kufundishia kama nukta nundu, tarakilishi, vichapishi vya nukta, kamera za usalama, nundu na makaratasi ya nukta nundu na kalamu ambavyo vina mchango mkubwa katika ufaulu wa wanafunzi.
- Uwekezaji katika mafunzo ya walimu utaimarisha uwezo wa walimu kufundisha katika shule jumuishi.
- Wanafunzi wenye changamoto za uoni watajifunza kwa ufasaha zaidi wakiwa katika shule maalum kuliko katika shule jumuishi.
- Ikiwa changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye changamoto za uoni, kama mazingira yasiyo rafiki ya kujifunzia, upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ujuzi usioridhisha wa walimu kufundisha zitafanyiwa kazi basi shule jumuishi zitachangia ufaulu wa kuridhisha kwa kundi hili la wanafunzi.
- Changamoto ya walimu kutokuwa na ujuzi wa kufundisha wanafunzi wenye changamoto za uoni wakiwa darasani ni kikwazo kwa wanafunzi kujifunza.

6.0. Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti, mapendekezo kadhaa yalitolewa kwa makundi tofauti ya wadau.

6.1. Mapendekezo kwa serikali

- Walimu wa shule za msingi na sekondari wapatiwe mafunzo yatakayowawezesha kuwa na ujuzi wa kufundisha katika darasa jumuishi.
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itayarishe mafunzo maalum na ya lazima kwa ajili ya kuwawezesha walimu kumudu elimu jumuishi, mfano, mafunzo ya lugha za alama na nukta nundu.
- Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye changamoto ya uoni vitengenezwe kwa ubunifu unaokidhi mahitaji yao.
- Wastani wa mwalimu kwa mwanafunzi katika darasa jumuishi uzingatiwe na upunguzwe.
- Idadi ya shule jumuishi ziongezwe.
- Maafisa elimu wa wilaya na mikoa wapewe mafunzo kuhusu mpango wa elimu jumuishi.
- Kuongeza fedha za kujikimu kwa shule jumuishi
- Kuwa na wataalumu wa kutengeneza vifaa vya wanafunzi wenye changamoto za uoni shuleni.

6.2. Mapendekezo kwa shule

- Ukaguzi wa mazingira ya shule ufanyike mara kwa mara ili kuondoa vikwazo vinavyosababisha wanafunzi wenye changamoto za uoni kutembea kwa shida katika maeneo mbalimbali ya shule.

- Kuhakikisha wanafunzi wenye changamoto za uoni wanashiriki ipasavyo katika shughuli za nje ya darasa.
- Walimu wajifunze na watumie mbinu bunifu kuwawezesha wanafunzi wenye changamoto ya uoni kuonyesha maarifa na uwezo wao.
- Wanafunzi wenye changamoto za uoni wapatiwe mahitaji maalum ikiwemo kuongezewa muda wa kufanya mitihani.
- Vifaa vinavyotumiwa na wanafunzi wenye changamoto za uoni vihifadhiwe vizuri,

  Kumbukumbu za wanafunzi wenye changamoto za uoni zihifadhiwe vizuri.

6.3. Mapendekezo kwa wazazi na walezi

- Kutembelea shule mara kwa mara kama njia ya kufuaitilia maendeleo ya watoto wao wenye changamoto za uoni ili kutambua changamoto zinazoweza kujitokeza.